Teacher.co.ke

**KISWAHILI**
**MUHULA WA PILI 2024**
**KIDATO CHA PILI**
**MUDA: SAA 2:30**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

***1. Ufahamu***

a. Shughuli za kimataifa zilitatizika kwa njia zisizomithilika (1x1=1)

b. Wahudumu wa afya walikosa nafasi ya matibabu au nafasi ya kulazwa katika hospitali wanazohudumu wenyewe. (1x1=1)

c.

1. Watu wengi kupoteza kazi zao.

2. Watu wengine kutuma kwa likizo bila malipo.

3. Wengine kukatwa mishahara kwa asilimia kubwa.

4. Biashara nyingi kufungwa nyingi zikipata hasara chungu nzima.

5. Benki kuathirika kwa wateja kushindwa kulipa mikopo. (3x1=3)

d.

1. Kukohoa

2. Kushindwa kupumua au ugumu wa kupumua

3. Joto jingi au baridi kali mwilini

4. Maumivu ya misuli au mwili,

5. Kutapika au kuendesha, kupoteza hisia za kuonja na kunusa (2x1/2=1)

e.

1. Kutovaa barakoa kila wakati unapoenda kwenye watu.

2. Kutokuosha mikono yako kwa maji yanayotiririka na sabuni au kuitakasa.

3. Kwenda kwenye mikusanyiko ya watu.

4. Kutozingatie umbali wa mita moja unapokumbana na watu. (3x1=3)

f.

1. Serikali ilitangaza kufungwa kwa shule.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

2. Kafyu ya saa moja usiku hadi saa kumi na moja asubuhi iliwekwa hapo awali

3. Kufungwa kwa uchukuzi wa kimataifa ulitangazwa

4. Kudhibitiwa kwa uchukuzi nchini kwa kupunguzwa kwa idadi ya watu kwenye uchukuzi wa uma.

5. Mikusanyiko ya watu ulipigwa marufuku

6. Kanisa kufungwa japo kwa muda.

7. Idadi ya watu katika arusi na mazishi kupunguzwa mno.

8. Maeneo ya burudani pia yalifungwa kwa muda (2x1=2)

g.

1. Saa za Kafyu zilipunguzwa

2. Uchukuzi wa kitaifa na kimataifa ulifunguliwa upya.

3. Shule pia zilianza kufunguliwa japo kwa watahiniwa.

4. Kufunguliwa kwa maeneo ya burudani

5. Maeneo ya kuabudu yalifunguliwa japo kwa masharti ya kiafya. (1x1=1)

h.

i) Kafyu

Amri ya kutotoka nje nyakati fulani haswa usiku hadi asubuhi kama ile ya usiku hadi asubuhi

ii) Mchakato

Hatua za kufuata wakati kufanya jambo kama hatua za kutafuta za kutafuta chanjo.

(2x1=2)

2. **UFUPISHO**

**(a) Athari za mfumko wa bei kwa wananchi. (maneno 35)**

i) Raia nchini wanalala nja
ii) Wananchi kutumia nusu ya mapato yao kununua chakula.
iii) Gharama ya maisha imepanda
iv) Familia nyingi zimeingia katika lindi la umaskini.
v) Wengi hawawezi kumudu bei ya bidhaa. ***(5×1=5)***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**(b) Mambo muhimu yanayozungumziwa na mwandishi katika aya za mwisho nne.(Maneno 55-60)**

i) Serikali haina uwezo wa kudhibiti vyanzo vya ongezeko la bei.
ii) Inapaswa kupanga mikakati fulani ili kukabiliana na hali hii.
iii) Wanasiasa wanapiga siasa bila kujali maslahi ya kimsingi ya wananchi.
iv) Baa la njaa limekuwepo na lipo nchini.
v) Familia nyingi zimeathirika kwani zinashindwa kumudu bei ya bidhaa.
vi) Serikali yapaswa kuchukua hatua ili kuhimili athari za mfumko wa bei.
vii) Gharama ya kupangisha nyumba ,maji,stima na mafuta imepanda.
viii) Kupanda kwa bei ya vyakula imesukuma familia katika umaskini.

(8x1=8)

***Ondoa nusu ½ alama kwa kila kosa jipya la sarufi hadi alama 3.***

***Ondoa ½ alama kwa kila kosa jipya la hijai hadi alama 3.***

***(utiriko 2)***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

3 **MATUMIZI YA LUGHA.(alama 40)**

a. i) ulimi na meno
ii) midomo (2x ½ =1)

b). pili (1x1=1)

c). Shadda ni mkazo unaowekwa katika silabi fulani ya neno ilhali kiimbo ni kupanda na kushuka kwa sauti mtu anapozungumza. (2x1=2)

d). i) kipashio kidogo cha lugha /neno kilicho na maana kisafuri (1x1=1)
ii) ki; ngeli
li; wakati/njeo,
cho; kirejeshi,
angu; mzizi,
kiw; kauli,
a; kiishio (6 x1/2 =3)

e) **Mustafa** alimwaga **maziwa** yote (1x2=2)
(kadiria majibu)


f). Mfano:
Paka amekunywa maziwa.
Kiima kiarifa ***(2×1=2)***

Mwanafunzi atunge sentensi yenye kitenzi kimoja.

g) Chakula kiliwatosheleza wanafunzi. (1x2=2)

h) Askari jela amefikishwa mahakamani.

Sentensi sahili




***(8 x ½ = 4)***

i). <u>Ku</u>cheza kwao kuliwafaa (wingi) ***(1×2=2)***
***(kadiria majibu)***

**j)** Mwanafunzi mtiifu sana alipewa zawadi jana jioni
mwanafunzi mtiifu;RN
mtiifu sana;RV
jana jioni; RE (3x1=3)
(Kadiria sentensi ya mwanafunzi)


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

k) **M**ama amewasili nyumbani. (mwanzoni mwa sentensi)
Usichome nyumba ya **R**idhaa.(mwanzoni mwa nomino za pekee)
Anapenda taasisi ya **TUKI**( kuandika akronimu)
Babu alisihi, '**M**heshimu watu wazima' (mwanzoni mwa usemi halisi) (2x1=2)

kumb : mifano ya sentensi sahihi ituzwe
maelezo bila mifano yasituzwe

l) Jiji hili lina majitu mengi. ***(1×2=2)***

m) Mwanafunzi asipotia bidii hatapita mtihani (1x2=2/0)

n). na jambazi; kiunganishi

wana; kumiliki ***(2×1=2)***

o) (i) Mji –makazi ya watu.

(ii) Mchi –kipande maalum cha mti kinacho tumika kutwangia vitu kwenye kinu.

(Atunge sentensi moja sahihi) ***(1×2=2)***

p) Juma alimtaliki Farida mwaka jana. ***(1×1=1)***

q) Mwalimu aliwaamkua wanafunzi wake. ***(1×2=2)***

r) Maadamu-kwa sababu
Mfano.
Zeraki walipongezwa maadamu wanawawezesha wengi kupata maarifa. ***(1×2=2)***

s) (i) kuzungumza ili kupitisha wakati

(ii) Kusema kwa mafumbo (2x1=2)

SARUFI-ondoa ½ alama kwa kila kosa baada ya kutuza.
HIJAI-Ondoa ½ alama hadi makosa 6 ***(6× ½ =3)***

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Sajili ya sheria; kuna msamiati maalum kama rufani

***(2×1=2)***

(b) X-Kiongozi wa mashtaka
Y-mshtakiwa ***(2×1=2)***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(c)

i) Lugha ya unyenyekevu na heshima; ikiwezekana mheshimiwa.
ii) Msamiati maalum-kukata rufani.
iii) Lugha dadisi-Ulisema unataka kukata rufani.
iv) Kubadili msimbo/kuchanganya ndimi-Umepata presidential amnesty.
v) Kuzingatia sarufi/lugha sanifu-Nitaenda kanisani kuabudu na kumshukuru Mungu.
vi) maswali na majibu; majina yako kamili? Mussa bin Maksuudi
vii) kunukuu vifungu vya sheria; kulingana na kifungu… ***(6×1=6)***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes